

## UJUMBE KWA WAZAZI NA WALEZI

Mpendwa wazazi na walezi,

Asante kwa msaada wako wote wakati wa wiki chache zilizopita hizi za kujifunza kwa mbali na kuweza kubadilika.

Kufuatia ushauri kutoka kwa Afisa Mkuu wa Afya, Serikali ya Viktoria imeshauri kwamba shule zinaweza kuanza kurudi kwa awamu kwenye mahali pa shulenii.

Katika **hatua ya kwanza**, wanafunzi wa Prep, Darasa la 1 na Darasa la 2, wanafunzi wa sekondari kubwa (Mwaka 11 na 12 VCAL na VCE) na wanafunzi wote katika shule za kitaalam watarudi shulenii kuanzia Jumanne (Tuesday) 26 Mei.

Wanafunzi wa mwaka 10 wanaofanya masomo ya VCE, pamoja na masomo ya VCE VET, wanapaswa pia kuhudhuria shule kwa masomo hayo panapowezekana. Ikiwa hii haiwezekani kwa mtoto/watoto wako, waalimu wetu watahakikisha kuwa kazi zinazotolewa kwa wanafunzi wanaohudhuria shulenii pia itatolewa mtoto/watoto wako.

Ili kuwasaidia wafanyakazi wote wa shule kuijandaa kwa mabadiliko haya, Jumatatu (Monday) Mei 25 itakuwa siku bila wanafunzi.

Katika **hatua ya pili** ya kurudi kwetu mahali pa shulenii, viwango vyote vya miaka mingine vitarudi tena shulenii kuanzia Jumanne (Tuesday) 9 Juni.

Kwa wanafunzi wale ambaa hawawezi kusimamiwa nyumbani na watoto walio katika mazingira hatarishi, mtindo uliopo wa masomo kwa mahali pa shulenii utabaki katika kipindi cha wiki mbili kuanzia Jumanne (Tuesday) 26 Mei hadi Jumanne (Tuesday) 9 Juni. Mchakato wa sasa tunaotumia kuwezesha wazazi na walezi kuonyesha siku au sehemu za siku ambazo masomo ya mahali pa shulenii yanahitajika yataendelea kwa kipindi hiki cha wiki mbili.

Wanafunzi wengine wote katika viwango hivi vya darasa na mwaka wataendelea kujifunza nyumbani hadi Jumanne (Tuesday) 9 Juni.

Mara tu kiwango cha mwaka kimerudi, wanafunzi wote watatarajiwa kuhudhuria shulenii kama kawaida. Hii inamaanisha ikiwa utachagua kubakiza mtoto/watoto wako nyumbani baada ya kiwango cha mwaka wao kurudi shulenii, hatuwezi tena kusaidia mafunzo yao nyumbani.

Hii haitumiki kwa watoto ambaa wanahitaji kutokuwepo kwa sababu za kiafya au za matibabu. Kwa familia hizo, tafadhali wasiliana nasi ili tuweze kupanga mpango unaofaa.

Njia hiyo hiyo inachukuliwa na shule zote za serikali huko Viktoria.

Ili kusaidia afya na ustawi wa wanafunzi pamoja na wafanyakazi wetu wote, shule yetu itaendelea na utaratibu ziada wa kusafisha na kutahimiza kuosha mikono mara mwingi.

Ikiwa mtoto wako ni mgonjwa au anahisi vibaya, anapaswa kutoenda shulenii. Anapaswa kubaki nyumbani na kutafuta ushauri wa matibabu.

Wakati Afisa Mkuu wa Afya ameshauri kuwa wanafunzi hawatahitajika kudumisha umbali wa mwili huko shulenii, kutakuwa na mabadiliko kadhaa muhimu kwa shughuli zetu za shule, kulingana na ushauri wa kiafya kwa shule zote unaopatikana hapa

<https://www.education.vic.gov.au/about/department/Pages/coronavirus.aspx>

Hii itatumika hadi tunapoeleza zaidi. Nitatoa maelezo zaidi juu ya mazingira ya shule yetu ya eneo haraka iwezekanavyo, lakini ni muhimu kutambua kuwa mabadiliko yatajumuisha:

- mipangilio ya marekebisho ya kuacha na kuchukua watoto, ikiwa pamoja na kupanga nyakati tofauti za kuanza na kumaliza shuleni;
- vizuizi kwa upatikanaji wa mahali pa shule kwa mtu yelete badala ya wafanyakazi wa karibu na wanafunzi wa shule;
- jinsi tunavyofanya mikutano na mahojiano kati ya mzazi na mwalimu

Tunaelewa kuwa familia zingine zinaweza kuhisi wasiwasi juu ya kurudi tena kwenye kufundisha na kujifunza darasani. Naweza kukuhakikishia kuwa uamuzi huu umeamuliwa kutegemea ushauri bora wa afya unaopatikana kwa serikali yetu.

Habari zaidi juu ya kurudi shuleni na virusi vya corona (COVID-19) inaweza kupatikana kwenye tovuti ya Idara, ambayo itaendelea kusashishwa:

<https://www.education.vic.gov.au/about/department/Pages/coronavirus.aspx>

Asante kwa msaada wako ulioendelea na uvumilivu wakati huu.

Tunatarajia kuwakaribisha wanafunzi wetu kurudi darasani.